

**HOTUBA YA**  
Ameer-e-Ahlesunnat Hazrat'e Allama Moulana Abu Bilal  
**MUHAMMAD ILYAS ATTAR**  
Qadiri Razavi دامت برکاتہم العالیہ

**UVIVU (KUGHAFILIKA)**  
**BOOKLET NO: 32 (NEGLIGENCE)**

**غفلت**

**DIBAJI**  
TOFALI LA DHAHABU  
HAYA ISIYO YA KAWAIDA  
WAJUMBE WATATU WA MAUTI  
MAKUCHA MACHONI NA MASKIONI  
MWILI WA MUHAMMAD IHSAAN  
ATTARI

Swahili Translation By  
Majlis Tarajim (Dawat-e-islami)

**HOTUBA YA  
AMEER – E – AHLESUNNAT SAYYIDNA ALLAMA MAULANA  
ABU BILAL MUHAMMAD ILYAS ATTAR QADIRI**

**UVIVU (KUGHAFILIKA)  
(NEGLIGENCE)**

**DIBAJI**

- **TOFALI LA DHAHABU**
- **HAYA ISIYO YA KAWAIDA**
- **WAJUMBE WATATU WA MAUTI**
- **MAKUCHA MACHONI NA MASKIONI**
- **MWILI WA MUHAMMAD IHSAAN ATTARI**

**UCHAPISHO WA MAJLIS MAKTABATUL MADINA**

**Swahili Translation By  
Majlis Tarajim (Dawat-e-islami)**

Hotuba Hii Ilitolewa Siku Ya Tatu Ya Kngamano La Dawat- E- Islami Katika Ahmadabad ( India) Mwaka 1418 A.H. Kuanzia Tarehe 28-30 Rajab- U Murajjab Sawia Na 28 – 30 Decemba 1997 - Ubaid Raza Ibn Attar ( Ameiandika) kwa Kiurbi.

**UVIVU**

Inshaa – Allah .....Kusoma Kitabu Hiki Kuta Kuwa Na Athari Kubwa Kwako.

Bwana Mtume..... Amesema , Enyi Watu Mwenye Kuniswaliya Kwa Wingi Hapa Duniani Ataepusha Na Maafa Mingi Na Hesabu Yake Siku Ya Kiyama Itakuwa Nyepesi.

**Firdaus – Ul- Akhbar Jarida 5 Uk 375 Hadith 8210 Darul Kutubul Arabiy Beirut.**

## TOFALI LA DHAHABU

Inasemekana Kwamba Mcha Mungu Mmoja Alipata Umiliki Wa Tofali La Dhahabu . Akazama Kimawazo Katika Kupenda Utajiri Wa Mali Na Akamaliza Wakati Wake Wote Kupanga Na Kupangua Namna Gani Atakavyo Tumia Hazina Yake Hiyo Mpya, Akawaza Vyakula Vitamu , Nguo Za kifahari na amezungukwa na kila aina ya wafanyikazi Tena Wakati Wote . Usiku Huo Akazama Ndani Ya Ndoto Ya Kifakhari Na Starehe Na Maisha Ya Hali Ya Juu Kabisa Na Akasahau Kabisa Na Kujawa Na Uvivu Katika Kumkumbuka Mola Wake ..... Alipotoka Nyumbani Kwake Asubuhi Na Huku Anawaza Ndoto Ya Usiku Aliyoota Alipata Karibu Na Ziara Ya Makaburi Ambapo Alimuona Mtu Aliyekuwa Anatengeneza Tofali La Udongo Kwa Kutumia Mchanga Wa Kaburi . Jambo Hili Lilimgutusha Na Kumuamsha Na Kumtoa Pazia Ya Sahau Na Uvivu Mbele Ya Macho Yake . Akaanza Kulia Na Kuwaza “Itakuwaje Wakati Watu Watatengeneza Matofali Ya Udongo Kutoka Kwenye Kaburi Langu Nitakapo Kufa ? Nyumba Zangu Za Kifakhari, Nguo Zangu Zakibwanyenye Zote Hizo Nita Zia Cha Hapa Duniani . Kudanganyika Na Tofali La Dhahabu Kunanipelekea Kwenye Uvivu Na Sahau . Ikiwa Nataka Kupenda Chochote Basi Lazima Iwe Ni Kwa Ajili Ya Allah..... Akaamua Kuachana Na Tofali La Dhahabu Na Kujilazimisha Maisha Ya Uchaji Mungu.

## YENYE KUSABABISHA UVIVU

Enyi Ndugu Wapenzi Waislam! Kwa Kusema Kweli Hasa Ni Kwamba Uvivu Huongezeka Pindi Mtu Anaponeemeka Kidunia . Usikubali Kuwa Mgonjwa Wa Uvivu Kwani Maradhi Haya Humuweka Mtu Mbali Sana Na Allah ..... Biashara Nzuri Ni Neema , Utajiri Ni Neema, Watoto Ni Neema lakini Kujishugulisha Zaidi Kwa Mambo Haya Kupita Kiasi Kutakutia Kwenye Uvivu.

Allah ..... Anasema Katika Sura Ya Al- Munafiquun:- Aya 9

Enyi Mlio Amin! .....

Yasikusahaulisheni Mali Yenu, .....

Wala Watoto Wenu, .....

Kumkumbuka Mwenyezi Mungu .....

Na Wenye Kufanya Hivyo Hao .....

Ndio Walio Katika Khasara .....

Aya Hiyo Inatupa Funzo Kubwa Sana Haswa Kwa Wale Ndugu Waliopewa Neema Pindi Wanapo Kumbushwa Kuhusu Swala Wao Kwa Haraka Hujibu “Niko Kazini , Hata Hii Kazi Ya Kutafutia Familiya Yangu Chakula Ni Ibaada , Nitakapo Pata Wakati Nitakuja Kujumuika Nanyi Huko Msikitini.” Uvivu Ndio Wenye Kusababisha Mtu Kusema Maneno Kama Hayo.

www.dawateislami.net



## KILIO CHA MFU HAKISAIDII

Watu Wenye Mawazo Ya Kulimbukiza Mali Hupata Taabu Ya Kusafiri Nchi Mbali Mbali Kwa Min- Aajil Ya Kupata Zaidi , Hawana Wasaa Wa Kuingia Msikitini , Hupoteza Pesa Nyingi Kwa Bidhaa Za Urembo Na Husahau Kutoa Angalau Kichache Kwenye Njia Ya Allah ..... Na Hutumia Ujanja Wa Aina Yoyote Kupata Pesa Bila Kujali Kuhusu Amali Njema . Lazima Watu Sampuli Hii Waamke Kabla Mauti Hayaja Wachukua Kutoka Kwenye Vitanda Vyao Vya Kifakhari Ndani Ya Nyumba Zao Zilizo Nawirishwa Na Kuwatumbukiza Ndani Ya Shimo La Giza Lililo Jaa Vijidudu Na Mabuibui Na Wakabakia Humo Wakipiga Makelele , ‘Ewe Alla ..... Nirudishe Duniani Angalau Nikuabudu Wewe , Nitatoa Mali Yangu Yote Kwa Ajili Yako , Nitaswali Swala Zote Tena Kwa Jamaa Na Kwa Takbira Ya Kwanza , Sitakosa Tahajjud (Swala Za Usiku ), Nitakaa Itikaf Msikitini, Nitafuga Masharafa Na Ndevu , Na Nitavaa Kilemba

( Kofia) Kichwani Wakati Wote , Ewe Alaah ..... Nirudishe Duniani , Nipe Nafasi Nyingine , Nitaondosha Mapambo Ya Uchafu Duniani Na Nitahubiri Mwenendo Wa Bwana Mtume ..... Kila Pahali , Ewe Allah ..... ! Nipe Nafasi Hata Kama Ni Chache Nitafanya Mambo Mengi Mema . Haya Makelele Ya Watu Walio Jishughulisha Na Anasa Katika Maisha Yao Hayata Wasaidia Lolote . Quran Takatifu Tayari Imeshawaonya Katika Sura Al- Munafiquun Aya 10-11 ;-

Na Toeni Katika Tulichokupeni .....  
Kabla Hayajamfikia Mmoja Wenu .....  
Mauti, Tena Hapo Akasema , Mola .....  
Wangu Mlezi ! Huniakhirishii .....  
Muda Kidogo Nipate Kutoa Sadaka .....  
Na Niwe Katika Watu Wema .....

Wala Mwenyezi Mungu .....  
Hataiakhirisha Nafsi Yeyote .....  
Inapofikia Ajali Yake , Na .....  
Mwenyezi Mungu Anazo .....  
Khabari Za Mnayo Yatenda .....

## HAYA ISIYO YA KAWAIDA

Hujjatul- Islam Imam Muhammad Ghazal.....  
Ndani Ya Mukashifatul Quloob Anaeleza kwamba, ‘ Mcha Mungu Mmoja .....  
Alikuwa Mgonjwa , Kwa Hivyo Nikamzuru. Nilikuta Wafuasi Wake Wengi Wamemzunguka Naye Analia , Nikamuuliza ‘ Ewe Sheikh ! Walia Kwa Sababu Ya Kuepukana Na Dunia ? Akajibu la Kwa Sababu Amekosa Swala Zake . Nikamuuliza ‘Vipi’ Umekosa Kuswali?’ Akajibu ‘Kila Niliposujudu Nilikuwa Mvivu , Kila Nilipoinua Kichwa Kutoka Kwenye Sijda Nilikuwa Mvivu Na Sasa Katika Hali Hii Ya Uvivu Ndiyo Ninaaga Nayo Dunia’. Kisha Akashusha Pumzi Mzito Sana Na Akasema Maneno Yafuatayo:-

- Ninawaza Kuhusu Kufufuliwa , Kuhesabiwa Na Nitakapokuwa Ndani Ya Kaburi Langu.
- Baada Ya Maisha Haya Ya Kifakhari Nitawachwa Peke Yangu Nikijitetea Kutokana Na Dhambi Zangu Na Mchanga Ndiyo Utakuwa Mto(Tandiko) Wangu .
- Ninawaza Kuhusu Hesabu Na Kitabu Changu Cha Amali
- Lakini , Ewe Muumba Na Mlezi Wangu! Matara Jio Yangu Yote Yako Kwako, Naamini Uwezo Ni Wako Wa Kunisamehe Madhambi Yangu.

**Mukashifatul Quloob Uk 22 Darul Kutub Ilmiyyah Beirut**

## **KULIYA WAKATI WA KURINGIA MOTONI**

Enyi Ndugu Wapenzi Waislamu! Tunapata Mafunzo Makubwa Sana Ndani Ya Hivi Viswa . Hebu Waangalie Hawa Wacha Mungu Waliopita . Kila Nukta Ya Maisha Yao Ni Kumkumbuka Allah ..... Na Walikuwa Wanyenyekevu Na Hawakujivuna Kwa Sababu Ya Ibada Zao, Lakini Walijawa na hofu ya kumuogopa Allah ..... Kwa Watu Waliozama Ndani Ya Uvivu, Hawa Na Hata Alama Ya Uchaji Mungu , Hata Alama Ya Ukweli Lakini Utaona Namna Wanavyo Jisifu Kuhusu Ibada Zao . Watu Wema Wa Allah..... Japokuwa Hulindwa Kutokana Na Madhambi , Wao Hutetemeka Kwa Khofu Ya Kumuogopa Allah..... Lakini Wenye Kuishi Ndani Ya Uvivu Wanadumu Ndani Ya Madhambi Na Wazi Wazi Wanadhihirisha Maovu Yao Na Wanayafurahia . Zinduka Na Utanabahi! Hujjatul Islam Muhammad Ghazali .....Anatuarifu Kwamba Sayyidna Abdulla Ibn Abbas ..... Anasema ,’ Mwenye Kufurahi Pindi Anapo Tenda Dhambi Ataliya Pindi Atakapo Ingia Motoni.

**Mukashifatul Quloob Uk 375 Beirut**

## **ITAKUWAJE IMANI YAKO IKIKUPOTEA**

Hilo Ni Somo La Kutosha Kuzingatiwa Kwa Wale Wenye Kuona Raha Pindi Wanapo Danganya, Wanapo Angalia Sinema Na Sarakasi, Wanapo Sikiliza Miziki, Wanapo Udhi Hisia Za Waislam. Tutakuwaje Sisi Ikiwa Allah ..... Hayuko Radhi Nasi Na Tutakuwaje Ikiwi Tumemuudhi Mtume Wake ..... Na Imani Yetu Ikapotea Kutokana Na Kufurahia Kuasi Kwetu Kunako Sababishwa Na Uvivu Na Kutupelekea Kwenda Motoni ? Allah ..... Anatuonya Ndani Ya Quran Aya 82 Sura Tauba

Wawache wacheke kidogo.....

Watalia sana.....

## **WAJUMBE WATATU WA MAUTI**

Hujjatul Islam, Sayyidna Immam Muhammad Ghazali..... Anatuarifu Ndani Ya Mukashifatul Quloob Kwamba Sayyidna Yaquub..... Na Malaika Wa Mauti Sayyidna Izraeel..... Walikuwa Marafiki. Safari Moja Malakul Mauti Akamtembelea Sayyidn Yaquub..... Ambae Alimuuliza Umekuja Kunitembelea Au Kuchukua Roho Yangu?.Malakul Mauti Akamjibu Kukutembelea. Sayyidna Yaquub ..... Akasema Kabla Hujakuja Kuchukua Roho Yangu Nitumie Wajumbe Watako Niarifu,Malakul Mauti Akasema Kwamba Nitakutumia Mmoja Au Wawili. Sasa Pindi Malakul Mauti Alipokuja Kuchukua Roho Yake Sayyidna Yaquub.....Akamuuliza Ulikubali Utaniletea Wajumbe Kabla Kuchukua Roho



Yangu Wako Wapi? Sayyidna Izraeel.....Akamjibu Tumekuletea Nyele Nyeupe (Mvi) Baada Ya Nyele Nyeusi Udhaifi Baada Ya Kuwa Na Nguvu Na Kijongo Baada Yakuwa Wima, Ewe

Yaquub ..... Hawa Ndio Wajumbe Tunao Watumia Watu Kabla Ya Kufa Kwao.

**Mukashifatul Quloob Uk21 Darul Kutubul Ilmiyyah Beirut**

Kuna Maonyo Makali Sana Ndani Ya Misemo Miwili Ifuatayo Ya Kiarabu;

Zama na Siku Zimepita Madhambi Yamekithiri .....

Mjumbe Wa Mauti Amewasili

Moyo Bado umeghaflika.....

Anasa Zako Za Dunia Ni Hadaa Ambazo Utajuta Kwazo.....

Matamano Yako Ya Kuishi Milele Duniani Ni Upuuzi.....

## **UGONJWA NI MJUMBE WA MAUTI**

Enyi Ndungu Wapenzi Waislam Tumefahamu Sasa Kwamba Malaika Wa Mauti Hutumia Wajumbe Kabla Mauti Kuja,Wako Wajumbe Wengine Mbali Na Wale Ambao Wameshatajwa: Maradhi, Upungufu Wa Nguvu Za Macho, Matatizo Ya Maskio Pia Ni Baadhi Ya Wajumbe Wa Mauti.Wajumbe Wa Sayyidna

Izraeel ..... Tayari Wameshatutembelea Wengi Wetu Sasa Tutasema Nini Kuhusu Uvivi! Wakati Nyele Zinapokuwa Nyeupe Na Tunajua Huyu Ni Mjumbe Wa Mauti Mtu Bado Hakubali Na Anakuambia Weupe Wa Nyele Umesababishwa Na Mafua (Flu)! Wakati Mtu Anapougua , Anajua Kuwa Huyu Ni Mjumbe Wa Mauti Bado Anakuwa Mvivu , Anasahau Kwamba Ugonjwa Unauwa Watu Wengi Kila Siku . Maradhi Yale Madogo Yanaweza Kuzidi Na Kusanbabisha Kifo, Halafu Wapenzi Wake Wanabaki Kulia Maadui Zake Wanafurahia Na Yeye Mwenyewe Anatumbukizwa Ndani Ya Shimo Lenye Giza Na Kufinikwa Kwa Mrundo Wa Mchanga Akibaki Pekee , Yeye Na Amali Zake

( Mzuri Au Mbaya).

## **JINA JUU YA MLANGO WA MOTONI**

Zinduka! Yeyeto Mwenye Kuishi Ndani Ya Uvivu Na Kudumu Katika Madhambi Amepotea Na Anamangamanga Kwenye Giza La Uovu Na Akifaulu Kupata Ghadhabu Za Allah ..... Na Mtume Wake ..... Atanaswa Ndani Ya Adhabu Za Akhera Mahali Ambapo Ma Juto Na Kutubu Hakutamsaidia Tena . Bado Unayo Nafasi , Haraka , Tubia Kikweli Kweli Na Uamue Kuishi Kulingana Na Mafundisho Ya Mjumbe Wa Allah ..... Bwana Mtme ..... Anasema “Yeyote Mwenye Kukosa Kwa Kusudi Swala Moja Jina Lake Huandikwa Kwenye Mlango Wa Moto Atakao Ungia”.

**Hilyatul Auliya Jarida 7 Uk 299 Hadith 10590 Darul- Kutubul Ilmiyyah Beirut.**

Riwaya Nyingine Inasema :-

“Ikiwa Mtu Akakosa Swaum Moja Ya Ramadhan Bila Sababu Za Kisheria , Hata Akifunga Baadaye Siku Zozote Atakazo Hawezi Kulipa Ile Siku Moja Aliyoiacha”.

**Jami Tirmizi Jarida 2 Uki75 Hadith 723 Darul Fikr Beirut.**

## **MOTO MACHONI**

Yeyote Mwenye Kutazama Wanawake Kwa Matamania , Mwenye Kutazama Sinema, Kusikiliza Miziki Na Kusenganya Lazima Kutubu Papo Hapo Hujjatul Islam Imam Muhammad

Ghazali ..... Anasema , “Mwenye Kuyajaza Macho Yake Kwa Haraam, Yatajazwa Kwa Moto Siku Ya Kiyama”

**Mukashifatul Quloob Uk 10 Darul Kutubul Ilmiyyah Beirut.**

## **MSUMARI MACHONI NA MASKIONI**

Mwanachuoni Mashuhuri Wa Hadith Na Mfuasi Mkubwa Wa Shafii Allama Jalaluddin Suyuti Asha Shafiee ..... Anasema , ‘ Usiku Wa Miraj Bwana Mtume ..... Aliona Watu Walio Dungiliwa Msumari Ndani Ya Macho Yao Na Maskio Yao. Akaambiwa “Waliangalia Yale Ambayo Wewe Huangalii Na Walisikiliza Yake Ambayo Wewe Husikiliza ”.

**Sharhus – Sudoor Ukiti Darul Kutub Ilmiyyah Beirut.**

Kwa Hivyo Watu Wenye Kuangalia Haraam Na Kusikiliza Haram Watashindiliwa Misumari Ndani Ya Macho Yao Na Masikio Yao Tahadhari! Usiangalie Habari Kwenye T.V Kumbuka ! Ni Haraam Kwa Wanaume Na Wanawake Kuangaliana Kwa Matamania Na Kila Haraam Inakupeleka Motoni . ( Allah ..... Asitujaliye)

## **NYUSO ZA MAJUSI ( WENYE KUABUDU MOTO )**

Enyi Ndugu Wapenzi Waislamu ! Kunyoa Ndevu Na Kuzipunguza Kiasi Kisichojaa Kiganja Cha Mkono (Hanafi) Ni Haram. Sayyidna Imam Muslim..... Anatuelezea Kwamba Bwana Mtume ..... Amesema , “Punguzeni Masharubu Na Wacheni Ndevu Na Musijifanani Na Majusi”.

**Sahih Muslim Jaridai Uk 129**

Hadithi Hii Imeamsha Na Kuzindua Majivuno Ya Muislamu,

Ni Ajabu Kwa Mtu Kudai Yuwampenda Bwana

Mtume ..... Na Huku Matendo Yake Ni Sawai Na Yale Ya Maadui Wa Bwana Mtume .....

## **NI NANI UNASTAHIKI KUJISTIRI NAYE**

Enyi dada zangu Waislamu ! Sikilizeni! Kutofinika Miili Yenu Ni Haraam, Kuangalia Wanaume Kwa Jicho La Matamania Ni Haraam ( Wale Ambao Hurusiwi Kuolewa Nao) Na Kuna Kupelekea Kuingia Motoni . Mwanamme Lazima Ajiepushe Kumuangalia , Kuzungunza,na kuwa Faragha Na Watoto Wa Kike Wa Ami Zake Na Wajomba Zake Na Washangazi Zake Na Wa Mama Zake Wakubwa Na Wadogo Na Pia Dada Zake Mkeo. Sheria Hii Pia Inamuhusu Mwanamke Na Mwalimu Wake Wa Dini (Sheikh) Mwanamke Haruhusiwi Kubusu Mkono Wa Sheikh Wake, Harahusiwi Kushikwa Kichwa Chake Na Sheikh Wake. Wavulana Watengwe Na Wasihana Wanapofikia Umri Wa Miaka 9 Kwa Wasichana Na Maka 12 Kwa Wavulana.



## MAVAZI YALIYO KATAZWA

Bwana Mtume ..... Amesema “(Usiku Wa Miraj) Nimeona Ndimi Za Watu Zikikatwa Kwa Makasi , Nilipouliza Makosa Yao Jibril ..... Akanijibu “Walijipamba Duniani Kwa Mavazi Yaliyo Haramishwa”. Vile Vile Nilisikia Vilio Na Kelele Kutoka Ndani Ya Shimo Lililo Towa Harufu Ya Uvundo , Jibril ..... Akanielezea “Hao Ni Wanawake Walio Jipamba Duniani Kwa Yale yaliyo Haramishwa ”

**Tarikh Baghdad Jarida 1 Uk 415 Darul Kutub Ilmiyyah**

Zinduka ! Rangi Za Kucha Zinafunika Kucha Zako Basi Kusababisha Maji Kutopenya, Na Kwa Sababu Hii Udhu Wako Unakuwa Hau Kamiliki Wala Josho Lako Halikamiliki Hivi Basi Kufanya Swala Yako Baatwil . Ninawaomba Dada Zangu Wa Kiislamu Kuvaajababu Za Madani, Kufinika Viganja Vyao Vya Mikono Kwa Glovu Na Miguu Yao Kwa Soksi Na Kamwe Wasidhihirishe Viganja Vyao Na Nyayo Zao Kwa Waume Ambao Wanaruhusiwa Kuwaoa .

## KUKIDHI SWALA

Ikiwa Umekosa Swala Au Swaum Zako Za Faradhi Lazima Ujue Ni Ngapi Na Kisha Uzikidhi , Na Utubie Kwa Kuchelewa Kwako Kukidhi Swala Ndani Ya Kitabu Kiitwacho “Njia Za Kukidhi Swalah “ Ambacho Kinapatikana Katika Maktabatul Madina. Kitabu hicho Kina Kuelezea Nguzo Muhimu Kuhusu Suala La Kukidhi .

**INSHAA – ALLAH...**

Ndugu Nyote Waislamu Nyanyueni Mikono Yenu Na Museme Inshaa- Allah ..... Na Kutia Nia Madhubuti Kuwa “Kuanzia Leo Hatuta Kosa Tena Hata Swalah Moja”

( Inshaa- Allah..... “Hatuta Kosa Swaum Ya Ramadhan Hata Moja”

(Inshaa- Allah ..... ) “Hatuta Angalia Tena Sinema “

( Inshaa- Allah .....)

“Hatuta Sikiliza Miziki Tena “ ( Inshaa- Allah ) “Hatuta Nyoa Ndevu Zetu Tena (Hanafi) ( Inshaa- Allah.....)

“Hatuta Punguza Ndevu Kiasi Kisicho Jaa Kiganja Cha Mkono “ (Inshaa- Allah .....)

## BARAKA ZA DAWAT –E- ISLAM

Kila Mmoja Ni Bora Ajiunge Na Awe Katika Jumuiko La Dawat – E – Islam Kwa Maana Inshaa –Allah ..... Utafaulu Hapa Duniani Na Kesho Akhera . Wacha Nikupe Habari Kuhusu Mafanikio Ya Hivi Karibuni Ya Dawat – E – Islam. Inshaa- Allah ..... Itaujaza Moyo Wako Kwa Hamu Na hisia Nzuri Na Mwishowe Inshaa – Allah ..... Kuugeuza Kuwa Bustani Zuri La Madina.

## MWILI WA MUHAMMAD IHSAN ATTARI

Kijan Mmoja Kwa Jina Muhammad Ihsan Kutoka Eneo La Gulbahar Mji Wa Karachi Alijiunga Na Dawat – E – Islam Na Akawa Mfuasi Wa Sayyidna Ghous – E- Adham



..... Kutokana Na Mafunzo Niliyompa. Jambo Hili Lilileta Mabadiliko Ya Madani Ndani Yake . Alifuga Ndvu Kubwa Na Kuvaa Kilemba Cha Kijani Kibichi Ishara Ya Imaama Shareef. Alijifunza Kusoma Quran Katika Madrasatul Madina Na Akaanza Kuamrisha Watu Mambo Mema . Haukupita Mda Akaanza Kuumwa Na Shingo Na Kila Akitibiwa Ugonjwa Nao Huzidi Na Akajikuta Katika Hali Maututi.. Aliandika Wasia Wake ( Aliojifundisha Kutoka Kwa Namna Nilivyo Andika Wasia Wangu , Ambao Unapatikana Katika Maktaba Ya Madina ) Na Kumpa Kiongozi Wake Kabla Kufariki Kwake . Aliaga Dunia Akiwa Na Takriban Umri Wa Maka 35 Na Kuzikwa Katika Makaburi Yetu. Aliusia Ndugu Zake Waislam Kusoma Kwa Muda Wa Masaa 12 Karibu Na Kaburi Lake Na Walisoma.

Siku Ya Jumanne Tarehe 6 Jamadul Akhir 1418 (7- Octoba 1997) Miaka Karibu Mitatu Na Nusu Baada Ya Kifo Chake , Mwili Wa Ndugu Mwingine Muislam Uthman Attar Uliletwa Kwenye

Makaburi Hayo Kuzikwa. Baadhi Ya Wale Ndugu Waliokuja Kuzika Waliliendea Kaburi La Ihsaan Attar .....Kwa Min- Ajili Ya Kumuombea Dua Lakini Kwa Mshangao Mkubwa Waliona Kuna Tundu Kubwa Pembezoni Mwa Kaburi Lake . Kiasi Kwamba Mtu Yuwaona Mpaka Ndani , Waliuona Mwili Wa Marehemu Muhammad Ihsaan Attari Aliyezikwa Miaka Mitatu Iliyopita Bado Haujaoza , Kilemba Chake Bado Kipo Kichwani Mwake , Na Sanda Yake Bado Yanukia Mafuta Mazuri . Habari Hii Ilienea Kwa Haraka Sana Usiku Huo Na Watu Walikwenda Kumtizama Marehemu . Miungoni Mwa Waliokuwepo Ni Wale Ambao Walikuwa Waki Fahamu Kimakosa Kuhusu Mambo Ya Dawat – E- Islami Na Baada Ya Kushuhudia Kisa Hichi Na Kuona Rehema Za Allah .....Kwa Ndugu Yao ( Marehemu ) Waliamua Na Kubadilisha Mawazo Yao Na Kujiunga Na Dawat – E – Islam.

## **MASHAHIDI WA DAWAT - E – ISLAM**

Enyi Ndugu Wapenzi Waislam ! Pengine Mumeshapata Habari Kuhusu Jaribio La Kumuuwa Mtumishi Mtakatifu Mnyenyekevu Wa Dawat- E – Islam Sunnah Tarehe 25 Rajab 1416 Katika Mji Wa Lahore . Matokeo Yake Ni Kwamba Muballigheen Wawili , Haji Uhud Raza Attari Na Muhammad Sajjad Attari ..... Walikufa Mashahidi . Baada Miezi 18, Mji Wa Lahore Ulikumbwa Na Mvua Kali Ambayo Ililiharib Kaburi La Haji Uhud Raza

Attari ..... Ikaamuliwa Kuchimbwe Kaburi Lingine Na Mabaki Yake Yazikwe Huko. Kwa Mshangao Waliupata Mwili Wa Marehemu Bado Hauja – Oza Wala Hauja Guswa Na Chochote . Mwili Huo Uligurishwa Na Kisa Hichi Kilishuhudiwa Na Watu Wengi Sana. Habari Hii Imeelezwa Kwa Kirefu Sana Ndani Ya Kitabu “Baraka Za Dawat–E- Islam “Sehemu Ya Pili . Ninawaomba Ndugu Na Dada Wote Wa Kiislamu Kujumuika Kwenye Mazingira Ya Dawat-E-Islam. Hakuna Mambo Ya Kujisajili Katika Dawat–E–Islam. Hudhuria Mikusanyiko (Ijtimah) Za

Dawat–E–Islam Kila Wiki Karibu Na Pale Unapoishi Na Mutoke  
( Kutembelea ) Pamoja

Na Ndugu Zako Ndani Ya Ashiqaan – E – Rasuul Ya Madani Qafila Upate Akhlaq (Tabia) Kulingana Na Sunnah . Kila Mtu

Ajaribu Uwezo Wake Kufundisha Mienendo Ya Sunnah Na Kuwalingania Wengine Katika Kutenda Mambo Mema Kwenye Kazi Zao, Biashara Zao Na Hata Mashamba Yao .

### **IJTIMA**

HUDHURIA KONGAMANO LA WIKI IJTIMAH LA DAWAT E- ISLAMI BILA KUCHELEWA KATIKA MIJI YENU NA UPATE BARAKA ZA SUNNAH. KATIKA MIJI WA MOMBASA KONGAMANO LA WIKI IJTIMAH LINA ANZA KILA IJUMAA BAADA YA SWALA YA MAGHRIB KATIKA MADANI MARKAZ (MASJID KANZUL IMAN) DAWATE ISLAMI – AREA TONONOKA MVITA.

### **BAADA YA KUSOMA KITAB HIKI MPE MWENZAKO**

Eneza Vitabu Vinavyo Chapishwa Na Maktabatul Madina Kwenye Sherehe Za Ndoa, Wakati Wa Misiba, Wakati Wa Ijtimai Na Hata Nyakati Zingine Na Ujipatie Thawabu . Ifanye Ni Ada Kuweka Vitabu Hivi Kwenye Biashara Zako Kwa Min-Ajil Ya Kuwagawanyia Bila Malipo Wateja Wako. Wape Wauzaji Magezeti Vitabu Hivi, Au Wape Watoto Wavieneze Kwa Majirani Zako Peana Kitabu Kila Wakati Na Upate Fadhili Za Kuamrisha Mema .

[www.dawateislami.net](http://www.dawateislami.net)

[www.dawateislami.net](http://www.dawateislami.net)